OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO
SHULE YA SEKONDARI MAFIGA
S.L.P. 6041 - MOROGORO
PHONE NUMBER: 0738- 268873

Jina la mwanafunzi ……

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAFIGA KIDATO CHA TANO 2022/2023

SHULE YA SEKONDARI MAFIGA NI SHULE YA KUTWA

Napenda kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mafiga iliyopo mkoani Morogoro katika Manispaa ya Morogoro. Ni shule ya kutwa ya wasichana na wavulana. Hongera kwa kupata nafasi hii. Umechaguliwa kujiunga na shule hii kwa masomo Sanaa katika tahasusi ya ……..

Utakuwa hapa shuleni kwa muda wa miaka miwili. Kwa kipindi chote utakachokuwa hapa shuleni, tutakuongoza na kukutunza ili uwe na mwenendo wa kufaa. Tunasisitiza, mzazi awe tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi kwa kutupa taarifa juu ya mwenendo wa mwanafunzi akiwa nyumbani.

Halikadhalika, kila mwisho wa muhula tutatuma maendeleo yako ya kitaaluma kwa mzazi/mlezi wako, tukitegemea kwamba ukiwa nyumbani wakati wa likizo utaendelea kuongozwa na kujisomea. Mzazi au mlezi tunategemea atatoa ushirikiano juu ya mwenendo wa mwanafunzi huyo. Tunasisitiza, uwapo shuleni, utatakiwa kuweka bidii na juhudi kubwa sana katika masomo ili uweze kufaulu vizuri mitihani yako ya kidato cha sita.

Mahali shule ilipo

Shule ya Sekondari mafiga, ipo katika kata ya Mafiga, Manispaa ya Morogoro, karibu na chuo cha kilimo SUA. Shule ipo umbali wa kilomita nne kutoka kituo kikuu cha mabasi Morogoro kiitwacho Msamvu. Nauli ya taksi kutoka Msamvu mpaka shuleni ni kati ya shillingi 5000/= na shilingi 6000/= tu. Vilevile usafiri wa mabasi madogo (daladala) unapatikana kutoka Msamvu hadi kituo cha daladala Mafiga kilichopo jirani na shule kwa kupitia katikati ya mji wa Morogoro kwa shilingi mia 400 tu.

Maagizo muhimu ya kuzingatia
Shule itafunguliwa kwa wanafunzi wote tarehe _____/2022. Tarehe ya mwisho ya kuripoti shuleni kwa wanafunzi wa Kidato cha tano ni _____/2022, baada ya tarehe tajwa, mwanafunzi atakuwa amepoteza nafasi hiyo. Mwanafunzi afikapo ataripoti ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa ajili ya kusajiliwa. Ni muhimu unapokuja shuleni ulete Hati halisi ya matokeo ya kidato cha nne (result slip) pamoja na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

A: MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

SARE ZA SHULE

Maelekezo kuhusu mshono, aina ya kitambaa na vipimo tazama hapa chini:

1. **WAVULANA**
   - Shati mbili “light blue tomato”
   - Suruali mbili zenye marinda mawili (upana chini sentimenta 16 pia iwe na “turn up” chini) rangi ya kijivu (dark blue).
   - Mkanda mweusi usiokuwa na ‘chata’ ya namna yoyote
   - Viatu vyeusi vyenye kamba (sio boot) na ambavyo havina visigino virefu
   - Soksi nyeupe jozi mbili (2)
   - Sweta moja bluu iliyokolea (Dark blue)
   - Tai moja inayopatikana shuleni rangi ya kijivu (grey)
   - Tisheti moja yenye nembo ya shule inayopatikana shuleni
2. **WASICHANA**
   - Shati mbili light blue tomato” mikono mifupi
   - Sketi mbili za kijivu zenye “ rinda boksi” moja mbele tu na yenye urefu usiopungua sentimita 15 kutoka kwenye goti kushuka chini.
   - Viatu vyeusi vyenye kamba ambavyo havina visigino virefu
   - Soksi nyeupe jozi mbili
   - Sweta moja la bluu iliyokolea (Dark blue)
   - Tai moja inayopatikana shuleni
   - Tisheti moja yenye nembo ya shule inayopatikana shuleni
   - Hijabu ndefu yenye kufikia kiunoni rangi “light blue”

     NB: Watakaohitaji kushonewa sare shuleni, waonane na uongozi wa shule kwa maelekezo zaidi.

B: MAHITAJI YA DARASANI

- Kalamu za kutosha za wino wa blue na nyeusi
- Daftari za kutosha (kaunta books quire three) dazani moja kwa ajili ya tini (notes)
- “ Mathematical set” kwa wale watakaosoma HGL na HGK

C: MICHANGO NA ADA

1. **ADA YA SHULE**
   - Ada ni Tsh.20,000/= kwa mwaka na mzazi /mlezi anaruhusiwa kulipa yote kwa pamoja ama nusu Tsh. 10,000/= kwa muhula mmoja.
   - Mwanafunzi unatakiwa kuandika jina kamili kwenye BANK PAY IN SLIP ili upewe stakabadhi ya shule.(zingatia cash money haipokelewi)
   - Shule hairuhusu matumizi ya hundi katika kulipa karo/ada au kulipia mahitaji mengine. Mzazi unashauriwa kukamilisha michango ya shule kwa wakati ili kuepuka usumbufu pia kuwezesha bajeti ya shule na serikali kutekelezeka kwa muda uliopangwa.

C: MICHANGO NA ADA.

1. **ADA YA SHULE**
   - Ada ni Tsh.20,000/= kwa mwaka, na mzazi /mlezi anaweza kulipa yote kwa pamoja au nusu Tsh. 10,000/= kwa muhula mmoja.
   - Mwanafunzi anatakiwa kuandika jina kamili kwenye BANK PAY IN SLIP.(Usilete pesa taslimu shuleni haitapokelewa).

2. **MICHANGO MINGINE**

- Taaluma …….20,000/=
- Dawati ……...45,000/=
- Umeme na maji ……10,000/=
- Michezo ……...3,000/=
- Ukarabati……10,000/=
- Huduma ya kwanza ….....10,000/=
- Walinzi na vibarua …….20,000/=

JUMLA…….118,000/=

Akaunti za Ada na michango ni:

Michango: 22103800031 NMB

Ada: 22101200115 NMB

Jina la Akaunti zote ni MAFIGA SECONDARY SCHOOL

D: VIFAA VYA KUFANYIA USAFI ANAVYOTKIWA KULETA MWANAFUNZI;

i. Bunda mbili rimu ya A4 kwaajili ya mitihani.
ii. Ndoo moja kubwa ya lita 20
iii. Wavulana; Kwanja 1 na fagio gumu (hard broom)
iv. Wasichana; Fagio la ndani 1 (soft broom) na chelelewa mbili.

E: SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Sheria zote za shule zimewekwa ili kuwawezesha wanafunzi kulifikia lengo la kuwepo kwao hapa shuleni kusoma na kuishi bila matatizo. Aidha sote tunaelewa kuwa nidhamu nzuri huleta mafanikio mazuri kitaaluma. Hivyo sheria utakazopewa hapa shuleni zimejikita katika misingi ya mambo makuu matatu:

- **Nidhamu**: Hii inamtaka mwanafunzi kufuata taratibu zote zilizowekwa na shule pamoja na Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kama mwanafunzi
- **Taaluma**: Hii inamtaka mwanafunzi kujibidisha katika kusoma kwa bidii ili kuleta heshima ya shule na mwanafunzi mwenyewe. Pia kuhudhuria vipindi vyote vya shule darasani na nje ya darasa, ifahamike kuwa kutoroka shuleni au vipindi ni kosa kubwa la kinidhamu.
- **Uvaaji wa sare za shule**: Hii inamtaka mwanafunzi anapokuwa shuleni kuvaa sare za shule zilizoidhinishwa na shule tu. Mavazi mengine nje ya sare zilizoidhinishwa na shule hazitavumiliwa kamwe.

TANBIHI:

Adhabu kali zitatolewa kwa wanafunzi wote watakaokiuka sheria za shule; simu, tablets, nguo za nyumbani, na vitu vingine visivyotakiwa shuleni vitachukuliwa na havitarudishwa na vyote vitaharibiwa mbele ya wanafunzi wengine.

G: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji, ushoga na ulawiti
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na biashara ya madawa ya kulevya
4. Makosa ya jinai
5. Kupigana
6. Kuharibu kwa maksudi mali ya uma na ya watu
7. Kudharau bendera na wimbo wa taifa
8. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani nan je ya shule
9. Kutoa au kushawishi kutoa mimba
10. Kuoa au kuolewa
11. Kugoma, kuchochea, na kuongoza na migomo na kuvuruga amani na usalama
12. Kukataa adhabu iliyotolewa na walimu
13. Utoro (kukaa nje ya shule zaidi ya siku tisini)
14. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani shuleni
15. Kuwa na simu ya mkononi, simcard, charger, vocha shuleni
16. Kutembelea nyumba za kulala wageni, bar, club, kumbi za starehe na sehemu zingiine ambazo kisheria mwanafunzi haruhusiwi

MWISHO

Natumia fursa hii kukukaribisha katika shule ya sekondari Mafiga na ni Matarajio yetu kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyopewa na Taifa lako.

.....

R. MARWA
MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI MAFIGA

C**. FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

- JINA LA MWANAFUNZI ----------
- TAREHE YA KUZALIWA ----------
- MAHALI ALIPOZALIWA/ MKOA/WILAYA ----------
- MNAISHI/MNAKA WAPI? ----------
- KATA/MTAA ----------
- URAIA MTANZANIA/SIYO MTANZANIA ----------
- SHULE ALIKOTOKA ----------
- NAMBA YA MTIHANI CSEE/(PSEE) ----------

TAARIFA YA WAZAZI/ MLEZI

- JINA LA MZAZI/MLEZI ----------
- KAZI YA MZAZI/ MLEZI ----------
- ANWANI YA MZAZI/MLEZI ----------
- SIMU YA MZAZI /MLEZI, KAZINI ----------
- NYUMBANI---------- MKONONI ---------- ---------
- KAMA HUNA SIMU ; NAMB YA SIMU YA JIRANI YAKO NI ----------
- BARUA PEPE (E-mail) YA MZAZI/MLEZI ----------

KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA

Mimi ---------- ---------- Kidato ---------- mwaka ----------

Nimeoma na kuyaelewa maelekezo yote, kwa hiyo nakubali kuipokea / sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa naahidi kuyazingatia.

Tarehe ---------- saini ----------

II; KUKUBALI SHERIA ZA SHULE
MWANAFUNZI

Mimi ---------- Nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi kwamba nitazizingatia na kutii masharti , sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na mwalimu/ waalimu na viongozi wote wa shule nikizikiuka sheria hizo hatua za kindhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni na taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe ---------- saini ----------

MZAZI/ MLEZI (Ajaze sehemu hii)

Mimi mzazi/ mlezi wake nathibitisha kuwa mwanangu …… ameelewa Maagizo. Mimi mzazi/mlezi ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni ---------- ------ na dhehebu lake ni ----------

Ninaruhusu/ siruhusu mwanagu kushiriki katika makongamano au warsha za kidini nje ya shule hususani zile zinazofanyika nje ya mkoa wa Morogoro pasipo kuwa na mwalimu mlezi wa shule hii.

Ninaruhusu/ siruhusu wakati wa likizo fupi atoke shuleni na kwenda kwa ---------- ---------- uhusiano wake na mwanangu ni ----------

Namba yake ya simu ni ----------

Aidha mimi ---------- ambaye ni mzazi / mlezi nimesoma/ nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu.

Mwanafunzi ---------- ninaahidi kutimiza wajibu wangu

nikiwa mzazi/ mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

---------- ----------

Jina la Mzazi/ mlezi **Sahihi ya Mzazi/ Mlezi**

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To the medical Officer

---------- (Name in full) please examine the named person as to his/ her physical and mental fitness for a full time student.

The examination should include the following categories (i) – (ii) each category of subcategory of which will render the applicant in eligible in case of defect Pregnancy (category iv) will also render a girl ineligible for students

(i) (a) Eye sight (b) Hearing (c)Speech (d) Limbs
(e) Venereal Diseases (f) Leprosy (d) Epilepsy

(ii) Neuroses

(iii) Other Serious Diseases

(iv) pregnancy

Date …… Signature ……

PART B

Medical certificate

(To be completed by the Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for a full-time student

(i) (a) Eye sight …… (b) Hearing …… (c)Speech ……
(d) Limbs ……
(e) Venereal Diseases …… (f) Leprosy ……

Epilepsy ……

(ii) Neuroses ……

(iii) Other Serious Diseases ……

(iv) Pregnancy ……

Station ……

Designation …… Signature ……

Date ……

A-LEVEL BOOKS REQUIREMENTS

GEOGRAPHY PAPER I:

(i) Monk House (1975). Principles of Physical Geography
(ii) Msabila DT. A comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School
(iii) John Pritchard (1990). Practical Geography for Africa.
(iv) Colin Buckle (1978). Land forms in Africa: An Introduction to Geomorphology.
(v) Bunnett, RB (2014). General Geography in Diagrams.
(vi) Francis Mnyawi(2014). Practical Geography for A-Level
(vii) David Waugh. An Integrated Approach to Geography.
(viii) D.N. McMaster. Map Reading for East Africa.

GEOGRAPHY PAPER II:

(i) Goh Cheng & Morgan. Human and Economic Geography
(ii) Tanzania Institute of Education. Advanced Level Geography Course book
(iii) Msabila, D.T (2014). An Integrated Regional study on Human and Economic Geography

ENGLISH LANGUAGE 1

(i) Asheli, N.E. A Practical Approach
(ii) Kadeghe, M. An Introduction to Language Advanced Level.

ENGLISH LANGUAGE 2

A. **NOVELS AND SHORT STORIES**:

(i) Chinua Achebe: A Man of the people.
(ii) Ayi Ewei Armah: The Beautiful ones are not yet Born.
(iii) Sago: His Excellency the Head of state.

B. **PLAYS:**

(i) Ngungi wa Thiong'o & Ngungi wa Mirii: I will marry when I want by
(ii)H. Ibsen: An Enemy of the people.
(iii)B. Bretch: The Caucasian Chalk Circle.
(iv)F. Imbuga: Betrayal in the City.
(v) Not Yet Uhuru
(vi) I Rwanda Magere
(vii) Black Mamba

C. **POETRY**:

(i) Tanzania Institute of Education: Selected Poems.
(ii) David Cook et. Al: Poems from East Africa

HISTORY:

(i) Rodney W., How Europe Underdeveloped Africa: Nairobi Heinemann Kenya (1992).
(ii) Nyirenda, H.D. Africa in World History. A-Level Certificate Notes DSM (DUP) 1992.
(iii) Nabudere, D.W. Essays on the Theory and Practice of Imperialism. DSM, THP (1979).
(iv) Lenin, V.I.(1982: Imperialism the highest stage of capitalism Moscow, Progress Publishers.
(v) Nyangwine, N. Advanced Level – History Notes, selected Topics for paper 1 & 2. (2002).
(vi) Fr. Jovitus F. Kimara Mwijage, Major Events in African History (2015)

KISWAHILI 1

(i)TET (2019) LUGHA NA SARUFI,Kiswahili shule za sekondari.Kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano na sita.
(ii)Kihore na Wenzake (2019)Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na vyuo.

(iii)Masamba na Wenzake (2006) Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na vyuo.

(iv) Mbunda M. (1992): Educational Publishers and Distributors Ltd, Dar es Salaam

(v) Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1958): Kiswahili Sekondari

(vi) James S. Mdee (1988): DUP

(vii) Oxford University Press (2012): Kiswahili Kidato cha Tano na Sita.

KISWAHILI 2

(i) Senkoro, F.E.M.K (2011): Fasihi

(ii) TUKI: Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Dar es Salaam. Toleo la Pili.

(iii). Morani. Emmanuel Mbogo. Macmillan AIDAN, DSM

(iv). Kwenye Ukingo wa THim. Ebrahim Hussein

(v)TET (2019)FASIHI.Kiswahili Shule za Sekondari.Kidato cha tano na sita.

Riwaya

(i) Kufikirika. Shaaban Robert. Mkuku na Nyota Publishers. Dar es Salaam, (2003)

(ii) Mfadhili. Hussein Tuwa. Macmillan AIDAN, (2007)

(iii) Usiku Utakapokwisha. Mbunda Msokile, Macmillan

(iv) Vuta Nkuvute. Shafi A. Shafi, Mkuki na Nyota Publishers, DSM (1999).

Tamthiliya

(i) Nguzo mama. Penina Mhando. Macmillan AIDAN, DSM (2007)

(ii) Kivuli Kinaishi. Said A. Mohamed. Oxford University Press

(iii) Morani. Emmanuel Mbogo. Macmillan AIDAN, DSM.

Ushairi

(i) Mapenzi bora. Shaaban Robert. Mkuki na Nyota Publishers (2007)

(ii) Chungu Tamu. T.A. Mvungi. THP DSM, (2000).

(iii) Fungate ya Uhuru. Mohamed Seif Khatib, DUP, DSM, (2000)

(iv) Kimbunga. Haji Gora Haji. TUKI, DSM (2003)

R. MARWA

Mkuu wa Shule